

JOHARI ALMASI
SHIRIKA LA UKUSANYAJI USHURU,
S. L. P. 574,
MWAMBAO.

21 – 05 - 2021

MWENYEKITI,
CHAMA CHA WAFANYABIASHARA,
S. L. P. 734,
MAPATO.

Kwa bi/bwana,

KUH: KUJADILI MANUFAA YA KULIPA USHURU

Ninachukua nafasi hii kukuandikia waraka nikiwa na matumaini kuwa u mzima. Madhumuni ya kuiandika barua hii ni kukualika pamoja na wanachama wako katika mkutano wa kujadili manufaa ya kulipa ushuru. Mkutano huo utafanyika katika afisi kuu za Shirika la Ukusanyaji Ushuru, hapa jijini Mwambao. Kikao kitaanza saa nne asubuhi, Jumamosi tarehe kumi Oktoba. Afisa mkuu wa forodhani nchini ndiye atakayekuwa mzungumzaji mkuu katika kikao hicho.

Tunaamini kuwa mtahudhuria ili tujifunze mengi. Ninaomba kukomea hapo. Ninawaomba afya njema na ufanisi katika biashara zenu. Pokeeni shukrani za dhati kutoka kwetu. Kwaherini.

Wako mwaminifu,

(sahihi)

Johari Almasi (katibu)